# OFISI YA RAIS

# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

# WILAYA YA UKEREWE

## MTIHANI WA KUJIPIMA WA KIDATO CHA PILI

**021** **KISWAHILI**

**MUDA Saa 2:30** **Mwaka: 2025**

---

**MAELEKEZO**

**1.** Mtihani huu una sehemu**A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi (10).**

2. Jibu maswali yote katika sehemu**A, B** na**C**.

**3.** Zingatia maelekezoya**kilasehemu**na**kilaswali.**

4. Andika kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

## SEHEMU A (Alama 15)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Chagua herufi ya jibu sahihi kuanzia kipengele (i) hadi (x) kasha andika herufi hiyo katika kisanduku ulichopewa.

i) Vipengele vifuatavyo hutumiwa katika uandishi wa barua rasmi isipokuwa …

A. Anuani ya mwandishi na mwandikiwa

B. Lengo

C. Kichwa cha barua/ mada

D. Saini najina la mwandishi

ii) Unyumbulishaji katika lugha ya Kiswahili huusisha upachikaji wa viambishi…..

A. Kabla ya mzizi wa neno

B. Katikati ya mzizi wa neno

C. Baada ya mzizi wa neno

D. Kabla na baada ya vitenzi

iii) Kiimbo hufasiliwaje katika mazungumzo?

A. Kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti

B. Kuzungumza kwa kupandisha mawimbi ya sauti

C. Kuzungumza na kuongea kwa sauti

D. Kuzungumza kwa kushusha mawimbi ya sauti

iv. Mzee Nkalango alipoulizwa swali la kutaja dhima nne za viambishi awali alitoa hoja tatu zilizo sahihi na hoja moja haikuwa sahihi. Ibainishe hoja ya Mzee Nkalango ambayo haikuwa sahihi miongoni mwa hizi zifuatazo;

A. Kudokeza njeo navitenzi

B. Kudokeza kauli mbalimbali za vitenzi

C. Kudokeza nafsi katika vitenzi

D. Kuonesha ukanushi

v. Sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuwepo kwa kizuizi chochote kwenye mkondo wa maneno hujulikana kama: -

A. sauti

B. Herufi

C. Irabu

D. Konsonanti

vi. Mimi ni hadithi fupi ninayoelezea makosa au maovu ya watu Fulani pamoja na kueleza maadili yanayofaa. Je mimi ni nani?
A.Ngano
B. Visasili
C. Vigano
D.  Soga

vii) Uundaji wa maneno nikitendo cha kuongeza maneno mapya katika lugha kwa kutumia njia mbalimbali. Je ni sababu zipi kati ya hizi zifuatazo haihusiki na uundaji wa maneno katika lugha?
A.Kukuza lugha katika jamii inayohusika
B.Kukidhi mahitaji ya mawasiliano
C.Kuibuka mambo mapya katika jamii
D. Kutofautisha uchumi na teknolojia katika jamii

viii) Dhima kuu ya ufahamu ni kuelimisha. Vilevile ufahamu una dhima zifuatazo isipokuwa
A.Ufahamu hukuza ustadi katika kusoma, kusikiliza na kutafakari kwa makini
B.Ufahamu huendeleza ujuzi wa lugha katika vipengele vya msamiati, sarufi na matumizi
C.Ufahamu husaidia kupata na kuongeza maarifa
D.Ufahamu husaidia katika kutambua miundo ya tungo mbalimbali

ix) Mojawapo ya alama za uandishi ni nukta.Kazi ya alama hiyo ni ipi katika hizi zifuatazo.
A.Kukariri au kurudia maneno yaliyosemwa
B. Kubainisha sehemu mbili za sentensi
C. kuashiria maneno yaliyo kwenye orodha
D.Kuonesha sentensi imefikia mwisho na imekamilika

x) Enzi za uhai wa Rais wa awamu ya pili ndugu Ali Hassan Mwinyi aliwahikusema “maishani kama **hadithi** jitahidi **hadithi** yako iwe nzuri pale utakapoondoka duniani” katika kauli hii, neon lililokolezwa wino linauhusiano na vipera vifuatavyo isipokuwa;

a) Tarihi

b) Visasili

c) Vigwano

d) Soga

**MAJIBU**

| i | ii | iii | Iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Oanisha vipengele katika **ORODHA A** na vipengele vilivyopo **ORODHA B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye visanduku ulivyopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| I. Mzizi<br>II. Mofimu huru<br>III. Kiambishi tamati<br>IV. Kiambishi cha kauli<br>V. Kiambishi awali | A. u-<br>B. -Chok-<br>C. esh-<br>D. ko-<br>E. Sasa<br>F. Oa<br>G. Mtoto |

**MAJIBU**

| I | Ii | iii | Iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

**SEHEMU B (ALAMA 70)**

**Jibumaswali yote katika sehemuhii**

3. Fafanua dhima za mofimu zilizokolezwa wino katika tungo zifuatazo. Tumia mifano kutoka katika maandishi husika kuonesha namna mofimu hizi zinavyoshiriki kuleta ujumbe na hisia kwa wasomi

i. Ame**ji**kata na kisu

______________________________

ii. A**me**tuongoza kwa muda mrefu sasa

______________________________

iii. **Ha**endi shuleni

______________________________

iv. **A**merudi kutoka shambani

______________________________

v. A**na**cheza mpira wa miguu

______________________________

4. Unganisha na tathmini tofauti zinazojitokeza kati ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Eleza vipengele vitanovinavyotofautisha lugha hizi, ukizingatia mifano ya matumizi katika muktadha wa kila moja.

i. ______________________________

______________________________

ii. ______________________________

______________________________

iii. ______________________________

______________________________

iv. ______________________________

______________________________

v. ____________________

____________________

5. Eleza muktadha wa rejesta zifuatazo kwa kutoa mifano ya kauli kwa kila moja. Hakikisha mifano yako inadhihirisha tofauti katika matumizi ya lugha kulingana na muktadha wa kijamii, kibiashara au kiserikali.

i. Ofisini

____________________

____________________

ii. Jikoni

____________________

____________________

iii. Bandarini

____________________

____________________

iv. Uwanjani

____________________

____________________

6. Changanua faida nne (4) za matumizi ya maneno mapya yanayotumika kati ya vijana wa kisasa katika kukidhi haja yao ya mawasiliano katika jamii.

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

IV.____________________

V.____________________

7. Mawasiliano ni muhimu miongoni mwa wanajamii na lugha ni mali ya jamii kama Nyenzo ya mawasiliano. Kwa mifano, eleza njia tano za kuondoa utata katika mawasiliano.

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

IV.____________________

V.____________________

8. a) Moja kati ya nyanja pana ni aina za maneno hivyo basi, kwa kutumia maneno yaliokolezwa rangi maalumu tunga sentensi kulingana na maelekezo uliopewa ya kila kipengele.

i) **Mimi** (litumike kama kiwakilishi)

______________________________________________

______________________________________________

ii) **Letu** (limtumike kama kivumishi)

______________________________________________

______________________________________________

iii) **Leo asubuhi** (litumike kama kielezi)

______________________________________________

______________________________________________

iv) **Upepo** (litumike kama nomino dhahania)

______________________________________________

______________________________________________

v) **Tumeshinda** (Litumike kama kitenzi)

______________________________________________

______________________________________________

b) Aina za maneno zimegawanyika katika makundi tofautitofauti, Chukulia wewe ni mwanafunzi wa Kiswahili uliebobea katika lugha hiyo. Wasaidie wanafunzi wenzako ambao hawazijui aina ya vivumishi katika sentensi zifuatazo.

i. Bata **maji** ni mtamu sana

______________________________

ii. Darasa **la nne** wamepata mfadhili

______________________________

iii. Pikipiki **mbovu** imekamatwa na Polisi

______________________________

iv. Mwanafunzi **mwenyewe** ni mtoro

______________________________

v. Watoto **wengi** wanapenda mayai

______________________________

9. a) Fafanua kwa upana dhana ya lugha

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b) Kwa kawaida binadamu tunawasiliana kwa kutumia lugha pamoja na vyombo vya mawasiliano, Chukulia umeenda kwenye jamii ambayo haitumii lugha, Ukiwa kama shahidi tuelezee changamoto ulizokutana nazo katika kijiji hicho.

i. ______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

ii. ______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

iii. ______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

iv. ______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

v. ______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**SEHEMU C (Alama 15)**

**Jibu swali la 10 katika sehemu hii**

10. Fasihi simulizi inahitaji vipengele maalum ili iwe hai na kuendelea kuhamasisha hadhira. Eleza vipengele vitano vya msingi vinavyohakikisha uhai wa fasihi simulizi na jinsi kila kipengele kinavyosaidia kuifanya fasihi hiyo iwe na nguvu na maana katika jamii. Toa mifano ili kuunga mkono hoja zako.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________